ELIMU YA MAZINGIRA

Tunaelewa kuwa majirani wetu ni washikadau muhimu katika jitihada zetu za uhifadhi wa wanyama pori na pia mazingira kwa ujumla ndani na nje ya hifadhi ya Ol Pejeta. Hii ikawa sababu ya msisitizo wa umuhimu wa elimu ya uhifadhi kwa wanaoishi katika jamii jirani. Kuafikia umuhimu huu, Ol Pejeta wamemuajiri afisa mpya wa elimu ya uhifadhi ambaye kazi yake ni kuongeza ufahamu kuhusu mazingira katika shule jirani na pia katika jamii.

MAJIRANI WAKARIBISHWA!

SHULE NA VIKUNDI KUTOKA JAMII JIRANI KUTEMBEA OL PEJETA BILA MALIPO!

KUTEMBELEA HIFADHI

Wanafunzi wa shule na vikundi tofauti vya jamii katika maeneo ya karibu na Ol Pejeta hupewa nafasi ya kutembelea hifadhi yetu bila malipo.
Wanaotaka kutembea huhitajika kupanga usafiri wao kisha kutuma ombi la kuzuru hifadhi ya Ol Pejeta kwa njia zifuatazo:

- Barua kwa: Head of Community Programs, Ol Pejeta Conservancy, Private Bag, Nanyuki 10400
- Barua pepe kwa cdp@olpejetaconservacy.org
- Ujumbe mfupi kupitia 0713 330 087

Maafisa wa hifadhi husaidia kupanga maelezo ya safari. Unapotuma ombi hakikisha kueleza yafuatayo; Jina la shule au kikundi, jamii unapoishi, tarehe ya ziara na idadi ya wanaonuia kutembea. Tunahimiza majirani wetu wote kutuma maombi ili wapate kutembea na kupata kuelimishwa.

HUDUMA ZA AFYA

Mwaka huu, Ol Pejeta imeweza kuboresha miundo mbinu katika kliniki ya Mwituria kwa ushirikiano na kilabu ya Rotary ya Langley, B.C na ile ya Nairobi Kaskazini. Kliniki hii, ambayo hutumikia zaidi ya watu 3,300 haijakuwa na nguvu ya umeme. Hali hii imezuia sana utoaji wa msaada wa dharura na kufanya uhifadhi wa chanjo na dawa kuwa tatizo kubwa. Ukarabati ulihusisha kuunganisha kliniki hii na nguvu ya umeme ili kuwezesha uhifadhi wa dawa na kuwawezesha wauguzi kuwahudumia wagonjwa wakati wa usiku. Uboreshaji huu pia umeongeza usalama katika kliniki kwa kutoa mwangaza wakati wa usiku. Bomba za ugavi wa maji pia ziliwekwa na kusambaza maji safi ya kisima ndani ya jengo.

MAWASILIANO KUPITIA SMS

Ol Pejeta inayo nambari ya ujumbe mfupi inayowezesha wanajamii kuwasiliana nasi moja kwa moja ilikufikisha habari na maoni. Usipige simu kwa nambari hii mbali ni ya ujumbe mfupi tu.

- Kwa maswali ya jamii ya jumla, tafadhali wasiliana nasi kupitia: 0790 889 940
- Ukiwa na ripoti muhimu inayohusu wanyama pori kuwa katika maeneo ya jamii, tafadhali wasiliana na ofisi yetu ya udhibiti (Control) kwa kupiga simu kwa nambari 0723 312 673

OL PEJETA CONSERVANCY

JARIDA LA HABARI

AUGUST 2017

TUZO LA USHINDI DUNIA NZIMA KWA KAZI YETU!

Aprili mwaka huu, Ol Pejeta ilishinda tuzo la jamii linalotolewa na World Travel and Tourism Council la Tourism for Tomorrow Community Award. Hili ni tuzo lililokuwa na ushindani mkali likihusisha mashirika zaidi ya mia mbili kote duniani. Tuzo hilo lilitunukiwa Moses Muthoki, Meneja wa Community Programs kwa niaba ya Ol Pejeta katika sherehe iliyofanyika kule Bangkok, Thailand. Kushinda tuzo hilo ni fahari kubwa inayoelezea mchango wa Ol Pejeta kwa jamii zinazoishi karibu na hifadhi. Mchango wa Ol Pejeta kila mwaka ni takriban dola milioni moja za marekani unaotokana na utalii na pia ufadhili kutoka kwa mashirika mengine. Akipokea tuzo hilo Bw. Muthoki alisifia wanajamii jirani na pia wafanyikazi wa Ol Pejeta kwa ushirikiano mwema na bidii katika kazi zao. Ol Pejeta imewekeza zaidi ya dola milioni 8 hadi sasa ilikusaidia mipango ya maendeleo ya jamii ikiwepo ni katika elimu, afya, kilimo na nishati safi.

TEKNOLOJIA YA KUOKOA NISHATI

Ol Pejeta na washirika Die Ofenmacher wanaendelea kutoa mazingira mbadala ya kirafiki kupitia majiko yaliyoboreshwa ya kupikia. Majiko haya yaliyoboreshwa hutumia kuni chini ya 70% chini ya majiko ya kawaida. Majiko haya pia huweza kupika vyakula viwili kwa wakati mmoja. Hivyo basi majiko haya huweza kuhifadhi mazingira kwa kupunguza ukataji wa miti, upishi wa mara kwa mara na uwezekano wa magonjwa yanayosababishwa na moshi. Mahitaji ya majiko haya kutoka kwa jamii yamekuwa ikiongezeka kwa kasi ndiyo sababu tumefundisha wanajamii 10 kuwa wajenzi wa majiko haya - ajira kamili. Mahitaji bado yanaongezeka hata hivyo, na sisi tunatarajia kuajiri wajenzi wengi zaidi wa majiko. Yeyote anayefurahishwa na mradi huu wanaweza kuwasili-ana nasi kupitia: bernard.mwangi@olpejetaconservancy.org au kwa simu kwenye nambari 0725 501 292.

TEKNOLOJIA KATIKA ELIMU

Katika kipindi cha miezi 6 iliyopita, Ol Pejeta imeboresha matumizi ya teknolojia katika shule jirani. Kupitia mradi huu, Ol Pejeta imetoa mafunzo ya utumizi wa tarakilishi katika shule 8 zilizoko katika jamii jirani. Hizi shule ni sekondari ya Tigithi, Thome, Sweetwaters, Ol Tafetta, Mwituria na St Augustine. Shule mbili za msingi ambazo ni Uwaso Nyiro na Irura pia zimefaidika. Kila shule imeunganishwa kwenye mtandao wa internet kwa ushirikiano wetu na shirika la Mawingu. Mradi huu utaendelea huku tukifadhili teknologia hiyo hiyo katika shule za upili za Malek, Tharua, Endana na Withare. Tunalenga kutoa elimu na vifaa vya ICT kwa shule zote katika eneo la jamii yetu kwa ushirikiano wa mashirika yakiwemo Paul G. Allen Foundation, Mawingu Networks, Afretech Aid Society na PA-MOJA. Tunapiga hatua kubwa katika kitengo hiki.

UFADHILI NA USHAURI

Kwa miaka kumi sasa, Ol Pejeta na washirika wenza, imewezesha zaidi ya wanafunzi 600 kupata elimu ya sekondari. Kama sehemu ya mpango huu wa ufadhili, tunatoa ushauri na mawaidha kwa wanafunzi wetu wanaofadhiliwa hasa wakati wa likizo. Wafanyikazi wa kitengo cha elimu katika Ol Pejeta huwezesha mikutano ya mashauriano kila muhula katika maeneo tofauti ya jamii zetu. Mikutano huhudhuriwa na wanafuzi na wazazi wao. Mpango huu huwapa wanafunzi fursa ya kutathmini mwelekeo wao shuleni na pia kuzungumzia na kutafuta mwafaka wa changamoto wanazokumbana nazo shuleni. Kadhalika, Ol Pejeta hukaribisha wasemaji mashuhuri kutoka sehemu tofauti duniani ilikunena na wanafunzi. Wanafunzi walionufaika na ufadhili huu siku za awali pia hujumuishwa kutoa wosia na kuwatia motisha wanafunzi wa sasa.

UKULIMA NA MAJI

Tumeshughulisha makundi kadhaa ya wakulima kupanda miti takriban 75,000 katika maeneo jirani na hifadhi na katika sehemu zilizo karibu na mito. Hii ni katika kusaidia uhifadhi wa mazingira kwa kuzuia mmomonyoko wa udongo na kulinda mito kama njia ya kuboresha uhifadhi wa mito. Ol Pejeta imebuni shughuli ya uhifadhi inayojulikana kama “Conservation in Action”. Shughuli hii inahimiza upandaji wa miti kupitia wanafunzi wa mashule yanayo tembelea Ol Pejeta. Ni shughuli inayowawezesha wanafunzi kujihusisha na uhifadhi na pia kuacha kumbukumbu ya ziara yao.
Kando na hayo kuna umuhimu wa watu wote kuteka na kuhifadhi maji nyumbani na shambani tukizingatia matukio ya ukame ambayo huikumba kaunti ya Laikipia. Kwa sasa, tumesaidia kuchimba vidimbwi vidogo vya maji 89 ambavyo wakulima wanatumia kwa ukulima wa mboga na kuwanywesha wanyama wanaowafuga.